



Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

**MUHTASARI WA MATOKEO YA
ROBO YA KWANZA (JANUARI - MACHI)
YA PATO LA TAIFA, 2017**



Ofisi ya Taifa ya Takwimu
Wizara ya Fedha na Mipango
Julai, 2017

1. Utangulizi

Pato la Taifa ni thamani ya bidhaa na huduma zinazozalishwa katika kipindi husika. Pato la Taifa kwa robo mwaka hutayarishwa katika kipindi cha miezi mitatu mitatu ambavyo ni Robo ya Kwanza (Januari - Machi), Robo ya Pili (Aprili - Juni), Robo ya tatu (Julai - Septemba) na Robo ya Nne (Oktoba - Desemba).


2. Matokeo Muhimu

Mwaka 2017, Robo ya kwanza ya Pato la Taifa kwa bei za miaka husika lilikuwa na thamani ya Shilingi trilioni 28.2 ikilinganishwa na Shilingi trilioni 25.8 zilizopatikana katika robo ya kwanza ya mwaka 2016.

Pato la Taifa katika robo ya kwanza ya mwaka 2017 kwa bei za mwaka 2007 lilikuwa Shilingi trilioni 12.7 ikilinganishwa na Shilingi trilioni 12.0 zilizopatikana katika kipindi kama hicho mwaka 2016. Pato la Taifa katika Robo ya kwanza ya mwaka 2017 liliongezeka kwa kasi ndogo ya asilimia 5.7 ikilinganishwa na asilimia 6.8 ya kipindi kama hicho mwaka 2016. Aidha, takwimu za awali za Pato la Taifa kwa robo ya kwanza ya mwaka 2016 zilionesha ukuaji wa asilimia 5.5.

Hata hivyo, shughuli za kiuchumi zilizokuwa na mchango mkubwa katika ukuaji wa uchumi kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2017 zilikuwa Uchimbaji Madini na Mawe zilizochangia asilimia 18.5, Ujenzi asilimia 15.9, Biashara na Matengenezo asilimia 11.8, Kilimo asilimia 10.6 na Habari na Mawasiliano asilimia 10.5.

Mchoro Na. 1: **Ukuaji wa Pato la Taifa Robo ya Kwanza ya Mwaka 2016 na 2017**




Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu, 2017

Ukuaji katika robo ya kwanza ya mwaka 2017 kwa baadhi ya shughuli za kiuchumi unaonesha kwamba, Shughuli ya Uchimbaji Madini na Mawe iliongezeka kwa kasi kubwa zaidi ya asilimia 35.3 ikifuatiwa na Habari na Mawasiliano iliyoongezeka kwa kasi ya asilimia 13.8 na shughuli za Ujenzi asilimia 8.4. Aidha, shughuli za kiuchumi za utawala na ulinzi ziliongezeka kwa kasi ya asilimia hasi 4.2 ikifuatiwa na shughuli za Uwakala katika Utawala **ambazo zilikua kwa kasi ya asilimia 1.1**. Shughuli nyingine za kiuchumi zilizokua kwa kasi ya kuridhisha ni pamoja na Fedha na Bima (asilimia 8.1), uzalishaji viwandani (asilimia 7.8) na biashara za jumla na rejareja (asilimia 6.8).

3. Ukuaji wa Uchumi katika Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC)

Ukuaji wa uchumi katika robo ya kwanza ya Mwaka 2017 mionganoni mwa Nchi za Afrika Mashariki, unaonesha kuwa, Pato la Taifa la Nchi ya Kenya liliongezeka kwa kasi ya asilimia 4.7 ikilinganishwa na asilimia 5.3 ya kipindi kama hicho mwaka 2016. Ukuaji wa Nchi ya Rwanda uliongezeka kwa kasi ndogo ya asilimia 1.7 robo ya kwanza ya mwaka 2017 ikilinganishwa na asilimia 8.9 ya kipindi kama hicho mwaka 2016. Uchumi wa Uganda uliongezeka kwa kasi ya asilimia 3.9 robo ya kwanza ya mwaka 2017 ikilinganishwa na asilimia 4.1 ya robo ya kwanza ya mwaka 2016. Ukokotoaji wa takwimu za Pato la Taifa kwa Nchi ya Burundi haujakamilika.

Mchoro Na. 2: Ukuaji Katika Asilimia Robo ya Kwanza (Januari – Machi) kwa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mwaka 2013 – 2017



Chanzo: Ofisi za Takwimu za Taifa Jumuiya ya Afrika Mashariki, 2017

4. Ukuaji wa Uchumi kwa Shughuli za Kiuchumi

4.1 Kilimo

Shughuli za Kilimo zinajumuisha uvunaji wa mazao ya mimea na wanyama, yanayotokana na uzalishaji wa mazao ya mimea, uzalishaji na ufugaji wa wanyama, uvunaji wa mazao ya miti kutoka katika mashamba ya miti pamoja na uvunaji wa wanyama pori na mazao ya miti ya porini.


Katika kipindi cha Januari hadi Machi, 2017, Shughuli za Kilimo ziliongezeka kwa kasi ya asilimia 2.6 ikilinganishwa na asilimia 2.7 ya kipindi kama hicho mwaka 2016. Kasi ndogo ya ukuaji ilisababishwa na kasi ndogo ya ukuaji wa sekta ndogo za misitu na uvuvi katika kipindi husika.

4.1.1 Kilimo cha Mazao

Mazao makuu ni pamoja na mahindi, mpunga, mtama/uwele, mazao mengine ya nafaka, mihogo, viazi mviringo, viazi vitamu, mazao mengine ya mizizi, maharage, mazao ya mafuta, mboga za majani, ndizi, mazao ya matunda, korosho, kahawa, pamba, chai, tumbaku na mazao mengine ya chakula na bishara.

Ukuaji katika shughuli ya uzalishaji wa mazao uliongezeka kwa kasi ya asilimia 3.0 katika robo ya kwanza ya mwaka 2017 ikilinganishwa na asilimia 2.7 ya kipindi kama hicho mwaka 2016. Kuongezeka kwa ukuaji kulitokana na upatikanaji wa mvua za masika zilizonyesha mwishoni mwa msimu katika baadhi ya maeneo ya uzalishaji Nchini.

Mchoro Na. 3: Uzalishaji wa Baadhi ya Mazao katika Robo ya Kwanza ya Mwaka 2016 na 2017



Chanzo: Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, 2017

Baadhi ya mazao makuu yaliyochangia katika ukuaji ni Mahindi asilimia 9.1 yaliyoongezeka kutoka tani elfu 1,577 katika robo ya kwanza ya mwaka 2016 hadi tani elfu 1,720 katika kipindi kama hicho mwaka 2017. Mpunga uliongezeka kwa asilimia 10.5 kutoka tani elfu 532 katika robo ya kwanza ya mwaka 2016 hadi tani elfu 588 katika kipindi kama hicho mwaka 2017. Maharage yaliongezeka kwa asilimia 7.9 kutoka tani elfu 508 robo ya kwanza ya mwaka 2016 hadi tani elfu 548 kipindi kama hicho mwaka 2017. Viazi mviringo viliongezeka kwa asilimia 6.9 kutoka tani elfu 29 katika robo ya kwanza ya mwaka 2016 hadi tani elfu 31 kipindi kama hicho mwaka 2017. Viazi vitamu viliongezeka kwa asilimia 11.1 kutoka tani elfu 27 robo ya kwanza ya mwaka 2016 hadi tani elfu 30 katika kipindi kama hicho mwaka 2017.

4.1.2 Mifugo

Uzalishaji wa mifugo na mazao yake unatokana na ufugaji wa mifugo ya kiasili na iliyoboreshwa. Mifugo hiyo ni pamoja na ng'ombe; mbuzi; kondoo; nguruwe; punda na farasi; sungura na kuku.

Ukuaji wa shughuli za mifugo ziliongezeka kwa kasi ya asilimia 2.7 katika robo ya kwanza ya mwaka 2017 ikilinganishwa na asilimia 2.6 ya kipindi kama hicho mwaka 2016. Ukuaji huu ulichangiwa na kuongezeka kwa wanyama waliovunwa pamoja na mazao yake ikiwa ni pamoja na maziwa na ngozi katika kipindi husika.

4.1.3 Misitu

Shughuli hii inahusika na uzalishaji wa mazo ya misitu, ikiwa ni pamoja na magogo, mkaa, kuni, na mazao mengine ya misitu yasiyotokana na miti kama asali na nta.

Ukuaji wa shughuli za misitu uliongezeka kwa kasi ya asilimia 1.5 katika robo ya kwanza ya mwaka 2017 ikilinganishwa na asilimia 4.3 ya kipindi kama hicho mwaka 2016. Kasi ya ukuaji wa shughuli hii ilipungua kutokana na Serikali kudhibiti uvunaji holela wa misitu.

4.1.4 Uvuvi

Shughuli ya uvuvi inahusika na uvunaji wa rasilimali za baharini na maji baridi, wenyе lengo la kuvua samaki na mazao mengine ya bahari.

Ukuaji wa shughuli za uvuvi uliongezeka kwa kasi ya asilimia hasi 1.9 katika robo ya kwanza ya mwaka 2017 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 1.2 kipindi kama hicho mwaka 2016. Kupungua kwa ukuaji wa shughuli hii ultokana na kupungua kwa uvunaji wa mazao ya baharini na maji baridi.

5.1 Uchimbaji Madini na Mawe

Uchimbaji madini na mawe unahusisha ukusanyaji wa madini yabisi yanayopatikana kwenye uso wa dunia (kama vile makaa ya mawe na chuma), vimiminika (petroli) au gesi (gesi asilia). Ukusanyaji huu unaweza kuwa chini ya ardhi, juu ya ardhi na pia kutoka kwenye visima. Shughuli hii inajumuisha pia kazi za ziada za kuongeza thamani ya madini kama vile kusafisha kukata na kupanga katika madaraja tayari kwa kupelekwa kwenye masoko.

Ukuaji wa shughuli hii uliongezeka kwa kasi ya asilimia 35.3 katika robo ya kwanza ya mwaka 2017 ikilinganishwa na kasi ya asilimia 6.5 katika kipindi kama hicho mwaka 2016. Ukuaji wa shughuli hii ultokana na kuongezeza kwa uzalishaji wa madini ya Tanzanite, chumvi, dhahabu, shaba na makaa ya mawe. Uzalishaji wa chokaa na makaa ya mawe ulikuwa mkubwa sana katika kipindi hiki.

Jedwali Na. 1: Uzalishaji wa Baadhi ya Madini Kipindi cha Januari – Machi, 2016 na 2017

Mineral	Kipimo	2016	2017
Tanzanite	Kg.	2,744	3,309
Chumvi	Tani	37,248	50,438
Gesi asilia	mmSFt3	11,980	11,388
Dhahabu	Kg.	10,596	10,698
Chokaa	Tani	262,451	927,973
Fedha	Kg.	4,162	3,488
Makaa ya mawe	Tani	38,704	128,685

Chanzo: Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania na Wizara ya Nishati na Madini, 2017

5.2 Uzalishaji Bidhaa Viwandani

Shughuli hizi zinajumuisha kuchakata malighafi kuwa bidhaa kwa ajili ya matumizi ya kati na ya mwisho. Bidhaa zinazotumika katika shughuli za uzalishaji viwandani ni pamoja na mazao ya kilimo, misitu, uvuvi, na bidhaa zinazotokana na uchimbaji madini na mawe.

Shughuli za Uzalishaji Bidhaa Viwandani ziliongezeka kwa kasi ya asilimia 7.8 katika robo ya kwanza ya mwaka 2017 ikilinganishwa na kasi ya asilimia 7.4 katika kipindi kama hicho mwaka


2016. Kasi ya ukuaji ilitokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa bidhaa za simenti, nguo shughuli za uchapishaji na bidhaa za usafirishaji na mitambo.

5.3 Uzalishaji Umeme

Uzalishaji wa umeme katika robo ya kwanza ya mwaka 2017 uliongezeka kwa kasi ya asilimia 4.4 kama ilivyokuwa katika kipindi kama hicho mwaka 2016. Ukuaji ulitokana na kuongezeka kwa umeme uliozalishwa hususan kutokana na gesi asilia.

Umeme uliozalishwa uliongezeka kutoka kWh milioni 1,752 mwaka 2016 hadi kWh milioni 1,785 kipindi kama hicho mwaka 2017 sawa na ongezeko la asilimia 1.9. Wakati huo huo, uzalishaji wa umeme katika mitambo ya TANESCO uliongezeka kwa asilimia 19.6, Uzalishaji kutoka Songas uliongezeka kwa asilimia 8.1, wakati uzalishaji wa umeme kutoka IPTL na wazalishaji binafsi ulipungua kwa asilimia 31.0 na asilimia 91.7 mtawalia.


Mchoro Na. 4: **Uzalishaji wa Umeme (Mill. Kwh) Kipindi cha Januari – Machi, 2016 - 2017**



Chanzo: TANESCO, 2017

Shirika la Uzalishaji wa Umeme (TANESCO) lilizalisha asilimia 76.5 ya umeme wote uliozalishwa. Kiasi kilichobaki cha asilimia 23.5 kilizalishwa na wazalishaji binafsi. Umeme uliozalishwa kwa kutumia gesi asilia ulichangia zaidi ya asilimia 62.6 ya umeme wote uliozalishwa katika kipindi hicho.

Mchoro Na. 5: **Umeme Uliozalishwa kwa Aina ya Vyanzo Kipindi cha Januari - Machi, 2017**




5.4 Usambazaji Maji

Shughuli ya kiuchumi ya usambazaji maji inahusika na kukusanya, kusafisha na kusambaza maji kwa ajili ya matumizi ya nyumbani. Shughuli hii inatekelezwa na Mamlaka za maji Safi na maji Taka za Miji na Manispaa hapa Nchini. Maji yanayosambazwa yanatumika pia katika kazi za uzalishaji wa mazao na mifugo.

Katika kipindi husika cha mwaka 2017, kiasi cha maji kilichozalishwa kiliongezeka hadi mita za ujazo milioni 55 kutoka Mita za ujazo milioni 54 zilizozalishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2016.

Ukuaji wa shughuli hii uliongezeka kwa kasi ya asilimia 2.0 katika robo ya kwanza ya mwaka 2017 ikilinganishwa na asilimia hasi 2.5 ya ukuaji katika kipindi kama hicho mwaka 2016. Ukuaji huu uliongezeka kutoptana na kuboreshwa kwa miundombinu ya kuzalisha na kusambaza maji mijini.

Mchoro Na. 6: **Kiasi cha Maji Kilichozalishwa Kipindi cha Januari - Machi, 2013 - 2017**



Chanzo: EWURA, 2017

5.5 Ujenzi

Shughuli ya ujenzi inajumuisha ujenzi kwa ujumla na shughuli maalumu za ujenzi wa majengo na kazi za kihandisi.

Shughuli hii iliongezeka kwa kasi ndogo ya asilimia 8.4 katika robo ya kwanza ya mwaka 2017 ikilinganishwa na asilimia 8.9 katika robo ya kwanza ya mwaka 2016. Ukuaji huu ultokana na kuendelea kwa miradi ya uwekezaji katika kipindi hicho. Baadhi ya miradi iliyochangia kukua ni pamoja na miradi ya ujenzi wa barabara katika makutano ya barabara ya TAZARA, barabara ya Dodoma - Babati, barabara ya Msimba - Ruaha - Mbuyuni na upanuzi wa kiwanja cha Ndege cha Mwanza. Viashiria vingine vya ukuaji wa shughuli za ujenzi ni pamoja na kuongezeka kwa uzalishaji wa saruji katika robo ya kwanza ya mwaka 2017 uliongezeka hadi kufikia tani 1,142,188 kutoka tani 690,640 zilizozalishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2016.

5.6 Biashara na Matengenezo

Shughuli hii inahusisha Uuzaji wa bidhaa za jumla na rejareja kwa aina yeote ya bidhaa, na utoaji wa huduma zinazohusiana na shughuli za kibiashara kwa ujumla. Pia inajumuisha matengenezo madogo madogo ya magari na matengenezo ya bidhaa za binafsi na kaya.

Shughuli ya kiuchumi ya uuzaaji bidhaa za jumla na rejareja pamoja na matengenezo iliongezeka kwa asilimia 6.8 katika robo ya kwanza ya mwaka 2017 ikilinganishwa na asilimia 5.8 kipindi kama hicho mwaka 2016. Ukuaji huu ulitokana na ongezeko la biashara ya uuzaaji wa jumla na rejareja zilizozalishwa ndani ya Nchi.

5.7 Uchukuzi na Uhifadhi

Shughuli hii inahusika na usafirishaji wa abiria na mizigo kwa njia ya reli, mabomba, barabara, maji na anga; pamoja na huduma za uhifadhi mizigo. Aidha, shughuli hii pia inajumuisha ukodishaji wa vifaa vya uchukuzi na madereva pamoja na usafirishaji wa barua na vifurushi.

Shughuli za uchukuzi na uhifadhi kwa robo ya kwanza ya mwaka 2017 zilikua kwa kasi ndogo ya asilimia 4.1 ikilinganishwa na kasi ya asilimia 7.9 katika robo ya kwanza ya mwaka 2016. Kasi ya ukuaji wa shughuli hii ilichangiwa na ongezeko la idadi ya abiria na mizigo iliyosafirishwa kwa njia ya reli na pia usafirishaji wa abiria kwa njia ya maji. Idadi ya magari ya abiria yaliyopewa leseni mwaka 2017 iliongezeka hadi kufikia 11,286 kutoka 10,648 mwaka 2016.

Jedwali Na. 2: **Usafirishaji wa Gesi Asilia na Abiria Kipindi cha Januari - Machi, 2016 - 2017**

Maelezo	Kipimo	2016	2017
Usafirishaji kwa Mabomba	mmSFt3	11,980	11,388
Abiria - Reli	Elfu	539	1,534
Usafirishaji abiria - Maji	Elfu	463	495
Mizigo - Reli	Tani Elfu	56	105

Chanzo: Shirika la Maendeleo ya Petroli, Shirika la Reli na SUMATRA, 2017

5.8 Huduma za Malazi na Chakula

Shughuli hii inahusika na utoaji wa huduma za malazi za muda mfupi kwa wageni na wasafiri wengine na utoaji wa huduma za chakula na vinywaji.

Shughuli ya huduma ya malazi na chakula katika robo ya kwanza ya mwaka 2017 ilikua kwa kasi ya asilimia 3.0 ikilinganishwa na asilimia hasi 1.3 robo ya kwanza ya mwaka 2016. Kasi ya ukuaji wa shughuli hii ilitokana na kuongezeka kwa idadi ya watalii wa nje kutoka 114,340 robo ya kwanza ya mwaka 2016 hadi 131,782 robo ya kwanza ya mwaka 2017.

5.9 Habari na Mawasiliano

Shughuli hii inahusika na uchapishaji vitabu na muziki, upigaji picha za video, uandaaji wa programu za video na runinga, kurekodi sauti, kuandaa na kurusha vipindi vya redio na runinga.

Shughuli za habari na mawasiliano katika kipindi husika cha mwaka 2017 zilikua kwa kasi ya asilimia 13.8 ikilinganishwa na asilimia 13.3 kipindi kama hicho mwaka 2016. Ukuaji huu


ulitokana na kuongezeka kwa muda wa maongezi kwa simu za mikononi na mezani na kupanuka kwa huduma za intaneti na utangazaji nchini kupitia vipindi vyatia redio na runinga.

5.10 Fedha na Bima

Shughuli hii inahusika na utoaji wa huduma za fedha na aina zote za bima, huduma za mifuko ya pensheni ya hiari na huduma nyingine za kifedha.

Shughuli za Fedha na Bima katika robo ya kwanza ya mwaka 2017 zilikua kwa kasi ndogo ya asilimia 8.1 ikilinganishwa na asilimia 13.5 kipindi kama hicho mwaka 2016. Kwa namba kamili (mchoro Na.7) ukuaji wa shughuli hii ulitokana na kuongezeka kwa kiwango cha amana kutoka wastani wa trilioni 17.6 mwaka 2016 hadi wastani wa trilioni 18.2 mwaka 2017; kuongezeka kwa kiwango cha mikopo kutoka wastani wa trilioni 15.6 mwaka 2016 hadi wastani wa trilioni 16.0 mwaka 2017; na ongezeko la huduma zinazotolewa na makampuni ya bima.

Mchoro Na. 7: Kiwango cha Amana na Mikopo Januari - Machi, 2016 na 2017



Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania, 2017

5.11 Upangishaji Nyumba

Shughuli hii inahusisha uuzaaji, ununuaji, ukodishaji na utoaji wa huduma nyingine za majengo kama vile kutathmini majengo. Shughuli hizi zinaweza kuendeshwa na mwenye jengo au kwa kukodisha na pia zinaweza kuendeshwa kwa kutoza ada au mikataba. Pia shughuli hizi zinajumuisha ujenzi wa miundo pamoja na umiliki au ukodishaji wa miundo hiyo.

Shughuli za upangishaji nyumba zilikua kwa kasi ya asilimia 2.3 robo ya kwanza ya mwaka 2017 sawa na ilivyokuwa katika kipindi kama hicho mwaka 2016. Ukuaji huu ulitokana na kuongezeka kwa mahitaji ya nyumba kwa ajili ya makazi hususan katika maeneo ya mijini.

5.12 Huduma za Kitaalam; Kisayansi, Ufundu na Huduma Nyingine

Huduma hizi zinajumuisha shughuli maalumu za kitaalamu, kisayansi na kiufundi. Shughuli hizi ni pamoja na huduma za kisheria, kihasibu, usanifu majengo na uhandisi; uchunguzi wa kiufundi, utafiti na maendeleo; matangazo na tafiti za kibiashara; huduma nyingine za mifugo; kukodi na kukodisha mali kupitia madalali, ajira, mawakala wa usafirishaji, usafirishaji watalii na

huduma za ulinzi na upelelezi; huduma za majengo na utunzaji mazingira; uendeshaji ofisi na shughuli nyingine zinazosaidia uendeshaji.

Shughuli hii ilikua kwa kasi ndogo ya asilimia 1.9 katika robo ya kwanza ya mwaka 2017 ikilinganishwa na kasi ya asilimia 6.0 katika kipindi kama hicho mwaka 2016. Ukuaji huu ultokana na kuongezeka kidogo kwa mahitaji ya huduma za kitaalamu; kisayansi, ufundi na huduma nyingine za kiutawala.

5.13 Huduma za Uwakala kwenye Utawala

Shughuli hii inajumuisha huduma mbalimbali zinazosaidia uendeshaji wa biashara kwa ujumla. Shughuli hizi ni pamoja na kukodi na kukodisha mali kupitia madalali, ajira, mawakala wa usafirishaji, usafirishaji wa watalii na huduma za ulinzi na upelelezi; huduma za majengo na utunzaji mazingira; uendeshaji ofisi na shughuli nyingine zinazosaidia uendeshaji.

Shughuli hii ilikua kwa asilimia 1.1 katika kipindi cha robo kwanza ya mwaka 2017 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 2.6 katika kipindi kama hicho mwaka 2016. Kasi ya ukuaji ilitokana na kuongezeka kidogo katika kipindi husika kwa shughuli za mawakala wa usafirishaji na wasafirishaji wa watalii Nchini na upangishaji majengo.

5.14 Utawala na Ulinzi

Shughuli hizi zinajumuisha kazi za kutunga na kutafsiri sheria, kazi za Bunge, ukusanyaji kodi ulinzi wa Taifa, usalama wa raia na mali zao, uhamiaji, usimamizi wa misaada kutoka nje ya Nchi na uendeshaji wa program mbalimbali za Serikali. Shughuli za mifuko ya pensheni pia sehemu ya Utawala na Ulinzi.

Shughuli hii iliongezeka kwa kasi ya asilimia hasi 4.2 katika robo ya kwanza ya mwaka 2017 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 23.9 kipindi kama hicho mwaka 2016. Ukuaji huu ultokana na kuondolewa katika sekta ya umma kwa wafanyakazi waliobainika kuwa na vyeti vya kugushi.

5.15 Elimu

Shughuli hii inahusika na utoaji wa elimu katika ngazi mbalimbali katika taasisi binafsi na za umma. Katika kipindi cha Januari hadi Machi, 2017 ukuaji uliongezeka kwa kasi ya asilimia 5.2 mwaka 2017 ikilinganishwa na asilimia 8.6 kipindi kama hicho mwaka 2016. Ukuaji huu ultokana na kuongezeka kwa wanafunzi waliodahiliwa katika shule za msingi na sekondari kwa mwaka 2017.

5.16 Afya ya Binadamu na Ustawi wa Jamii

Shughuli hii inajumuisha utoaji wa huduma za afya ya binadamu na ustawi wa jamii kwa watoa huduma binafsi na umma.

Ukuaji wa shughuli hii uliongezeka hadi kufikia asilimia 5.4 katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2017 kutoka asilimia 5.3 ya kipindi kama hicho mwaka 2016. Ukuaji huu ultokana na kuongezeka kwa huduma bora kutoka kwa watoa huduma wa binafsi na umma katika kipindi husika.

5.17 Huduma Nyingine za Jamii

Shughuli hii inajumuisha shughuli za vyama vya siasa, jumuiya mbalimbali za kijamii, matengenezo ya vifaa vya nyumbani ambavyo havijaaishwa katika shughuli zingine kiuchumi zilizotajwa. Pia imejumuishwa shughuli za Sanaa na Burudani na shughuli za Kaya kama Mwajiri.

Huduma nyingine za Kijamii zilikua kwa asilimia 6.4 katika kipindi cha robo ya kwanza mwaka 2017 sawa na ilivyokuwa katika kipindi kama hicho mwaka 2016. Ukuaji huu ilitokana na kuongezeka kwa mahitaji ya wakazi mijini na huduma za binafsi.

6.0 Hitimisho

Katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2017, kasi ya ukuaji wa uchumi iliongezeka kwa asilimia 5.7 ikilinganishwa na kasi ya asilimia 5.5 kwa takwimu za awali za mwaka 2016 na asilimia 6.8 ya takwimu zilizorekebishwa za kipindi kama hicho mwaka 2016. Shughuli za kiuchumi ambazo ziliongezeka kwa kasi kubwa ziliwu ni pamoja na Uchimbaji Madini na Mawe (asilimia 35.3); Habari na Mawasiliano (asilimia 13.8) na Ujenzi (asilimia 8.4).

